

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 62 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) APRILI 2026

TSC YAIMARISHA MATUMIZI YA MFUMO WA TEHAMA KUSIMAMIA TAARIFA ZA WALIMU



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, akifungua mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Walimu (TSCMIS) kwa Maafisa TEHAMA wa mikoa pamoja na watumishi wa TSC ngazi ya Makao Makuu na wilaya tarehe 31 Machi, 2026 katika Ukumbi wa OSHA jijini Dodoma.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

 Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania  [tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)

TSC Ipongezwe kwa Kuendelea Kuimarisha Matumizi ya Mfumo wa TSCMIS


Hatua ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kuendesha mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Walimu (TSCMIS) nijambola kupongezwa katika juhudi za kuimarisha utendaji wa sekta ya elimu nchini. Mafunzo hayo yaliyowakutanisha Maafisa TEHAMA wa mikoa pamoja na watumishi wa Tume kutoka Makao Makuu na wilayani yanaonesha dhamira ya dhati ya Tume kuhakikisha matumizi ya teknolojia yanatumika kikamilifu kuboresha utoaji wa huduma kwa walimu.

Mfumo wa TSCMIS una umuhimu mkubwa katika kurahisisha usimamizi wa masuala ya kiutumishi ya walimu. Kupitia mfumo huo, shughuli mbalimbali kama usajili wa walimu, utoaji wa namba za usajili, mikataba ya ajira, pamoja na kushughulikia mashauri ya nidhamu na rufaa vinaweza kufanyika kwa ufanisi na kwa uwazi zaidi. Hali hii inaongeza uwajibikaji na kusaidia kupunguza urasimu katika utoaji wa huduma.

Hata hivyo, mafanikio ya mfumo huu hayatategemea tu watumishi wa Tume bali pia ushiriki wa walimu wenyewe. Ni muhimu kwa walimu kuuelewa na kuutumia mfumo wa TSCMIS kwa kuwa unawahusu moja kwa moja katika masuala yao ya kiutumishi. Kupitia mfumo huo, walimu wanaweza kuwasilisha hoja, changamoto au maswali yao kwa Tume kwa urahisi zaidi na kupata majibu kwa wakati.

Aidha, inafaa kutambua mchango wa wadau mbalimbali waliofanikisha mafunzo haya, hususan Mradi wa Shule Bora, ambao umeendelea kushirikiana na TSC katika kujenga uwezo wa watumishi na kuimarisha usimamizi wa sekta ya elimu. Ushirikiano huu ni mfano mzuri wa namna taasisi za serikali na wadau wa maendeleo wanavyoweza kushirikiana katika kuboresha huduma kwa walimu na hatimaye kuinua ubora wa elimu nchini.

KATUNI



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti
Paulina M. Nkwama

Wajumbe
Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya
Edwin Mgendera
Apsa Othman
Asha Lubuva

Mhariri Mkuu
Artemony T. Vincent

Mhariri
Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa
Lucas G. Ogunde

Wasiliana nasi kwa Simu: +255 756 927 131 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, **S.L.P 353, DODOMA.**



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

TSC Yaimarisha Matumizi ya Mfumo wa TEHAMA Kusimamia Taarifa za Walimu



Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bi. Kainda Ndasa, akitoa neno la ukaribisho kwa washiriki wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa TSCMIS kwa Maafisa TEHAMA wa mikoa pamoja na watumishi wa TSC ngazi ya Makao Makuu na wilaya tarehe 31 Machi, 2026 katika Ukumbi wa OSHA jijini Dodoma.

Na Mwandishi Wetu - Dodoma

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeendelea kuimarisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kusimamia taarifa za walimu nchini, hatua inayolenga kuongeza ufanisi wa utendaji pamoja na kuboresha utoaji wa huduma kwa walimu.

Hayo yameelezwa na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama, wakati akifungua mafunzo ya siku tatu ya matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Walimu (TSCMIS) tarehe 31 Machi, 2026 katika Ukumbi wa OSHA jijini Dodoma.

Akizungumza katika ufunguzi wa mafunzo hayo, Mwl. Nkwama alisema mfumo wa TSCMIS umekuwa nyenzo muhimu katika kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Tume pamoja na kuongeza uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa huduma kwa walimu.

Alieleza kuwa tangu kuanza kutumika rasmi mwezi Machi mwaka 2023, mfumo huo umewezesha kurahisisha shughuli mbalimbali za kiutumishi ikiwemo usajili wa walimu, kushughulikia mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu, pamoja na utoaji wa namba za usajili, barua za ajira na

mikataba ya ajira.

"Matumizi ya mfumo huu yameboresha uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa huduma kwa walimu na kurahisisha utendaji wa majukumu ya Tume kuanzia ngazi ya shule, wilaya hadi Makao Makuu," alisema Mwl. Nkwama.

Aliongeza kuwa mfumo huo pia umeunganishwa na mifumo mingine ya Serikali ikiwemo Human Capital Management Information System (HCMIS), School Information System (SIS) wa TAMISEMI pamoja na Hazina yaani Treasury Pension Payment System (TPPS), hatua inayorahisisha ubadilishanaji wa taarifa muhimu za kiutumishi.

Aidha, aliwataka Maafisa TEHAMA wa mikoa walioshiriki mafunzo hayo kuhakikisha wanawajengea uwezo wenzao katika halmashauri ili matumizi ya mfumo wa TSCMIS yaweze kuimarika zaidi katika maeneo yao ya kazi.

Katika hatua nyingine, Katibu huyo alipongeza ofisi za halmashauri kote nchini kwa ushirikiano wanaoutoa kwa Tume katika kushughulikia masuala mbalimbali ya walimu.

Alisema kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura ya 448, Tume ina wajibu wa kufanya vikao vya mashauriano na ofisi za

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama (katikati), Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA wa TSC, Bi. Kainda Ndasa (kushoto) na Mratibu wa Mradi wa Shule Bora Mkoa wa Pwani, Bi. Patronia Kimizye, wakifuatilia matukio mbalimbali wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa TSCMIS jijini Dodoma.

Wakurugenzi wa Halmashauri pale inapohitajika, jambo linalosaidia kuimarisha usimamizi wa walimu katika ngazi ya halmashauri.

"Tunatambua mchango na ushirikiano wa halmashauri katika kusimamia walimu. Wito wangu ni kuendelea kudumisha ushirikiano huu ili kuhakikisha walimu wanapata huduma stahiki kwa wakati," alisema.

Mwl. Nkwama aliongeza kuwa Tume pia inalenga kuhakikisha walimu wanauelewa vizuri mfumo wa TSCMIS kwa kuwa unawahusu moja kwa moja katika masuala yao ya kiutumishi.

Alifafanua kuwa kupitia mfumo huo, walimu wanaweza kuwasilisha hoja, maswali au changamoto zao moja kwa moja kwa Tume ili ziweze kushughulikiwa kwa wakati.

Aidha, aliwashukuru wadau wa Mradi wa Shule Bora kwa kuendelea kushirikiana na Tume katika kufanikisha mafunzo hayo yanayolenga kuboresha usimamizi wa utumishi wa walimu nchini.

Mafunzo hayo yanawakutanisha Maafisa TEHAMA kutoka mikoa yote Tanzania Bara pamoja na watumishi wa TSC ngazi ya Makao Makuu na wilaya kwa lengo la kuongeza uelewa wa matumizi ya mfumo huo katika utoaji wa huduma kwa walimu.

TSC Yaimarisha Matumizi ya Mfumo wa TEHAMA Kusimamia Taarifa za Walimu



Baadhi ya washiriki wa mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa TSCMIS wakifuatilia hotuba ya ufunguzi wa mafunzo hayo ya siku tatu yanayowakutanisha Maafisa TEHAMA wa mikoa pamoja na watumishi wa TSC ngazi ya wilaya katika Ukumbi wa OSHA jijini Dodoma.

TSC Yaimarisha Matumizi ya Mfumo wa TEHAMA Kusimamia Taarifa za Walimu



Baadhi ya washiriki wa mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa TSCMIS wakifuatilia hotuba ya ufunguzi wa mafunzo hayo ya siku tatu yanayowakutanisha Maafisa TEHAMA wa mikoa pamoja na watumishi wa TSC ngazi ya wilaya katika Ukumbi wa OSHA jijini Dodoma.

TSC HAI YABAINISHA MAFANIKIO KATIKA USIMAMIZI WA UTUMISHI WA WALIMU

Na Mwandishi Wetu

Serikali kupitia Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeendelea kuimarisha sekta ya elimu kwa kutekeleza hatua mbalimbali zinazolenga kuboresha ajira, maslahi na mazingira ya kazi kwa walimu nchini.

Hatua hizo zimeanza kuonekana kwa vitendo katika maeneo mbalimbali nchini, ikiwemo Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro ambapo ofisi ya TSC imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2025.

Katika kipindi hicho, Serikali imeendelea kuweka mkazo katika kuboresha ustawi wa walimu kwa kuhakikisha upatikanaji wa ajira, maendeleo ya kazi pamoja na kushughulikia changamoto mbalimbali zinazoweza kuathiri utendaji wao kazini.

Akizungumza kuhusu mafanikio hayo, Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Hai, Bi. Sophia Abdallah Msangi, amesema jitihada za Serikali zimeleta mabadiliko makubwa katika sekta ya elimu, hususan kwa walimu wanaotekeleza jukumu la kuwalea na kuwaelimisha wanafunzi.

Amesema katika kipindi cha miaka minne iliyopita, Serikali imefanikiwa kuajiri jumla ya walimu 230 katika wilaya hiyo, ambapo walimu 75 wameajiriwa katika shule za msingi na walimu 155 katika shule za sekondari. Kwa mujibu wa Bi. Msangi, hatua hiyo imechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza upungufu wa walimu katika shule mbalimbali na kuboresha utoaji wa huduma ya elimu kwa wanafunzi.

Baada ya mwalimu kuajiriwa, maendeleo yake ya kiutumishi yanaenda hatua kwa hatua. Bi. Msangi amesema jumla ya walimu 268 wamethibitishwa kazini katika kipindi hicho, wakiwemo walimu 88 wa shule za msingi na walimu 180 wa shule za sekondari.

Aidha, amesema Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika kupandisha vyeo walimu wenye sifa

ili kuongeza motisha kazini. Takwimu zinaonesha kuwa jumla ya walimu 1,845 wamepandishwa vyeo katika wilaya hiyo, ambapo walimu 942 ni wa shule za msingi na walimu 903 ni wa shule za sekondari.

Amesema hatua hiyo imechangia kuongeza ari ya walimu katika kutekeleza majukumu yao ya kufundisha na kusimamia maendeleo ya wanafunzi shuleni.

Katika kuhakikisha walimu wanaostaafu wanapatiwa haki zao kwa mujibu wa taratibu za utumishi wa umma, Bi. Msangi amesema Ofisi ya TSC Wilaya ya Hai imetoa vibali vya kustaafu kwa walimu 143 waliotimiza masharti ya utumishi, wakiwemo walimu 135 wa shule za msingi na walimu 8 wa shule za sekondari.

Akizungumzia kushughulikia kero za walimu, amesema Serikali imepiga hatua kubwa katika kupunguza changamoto zilizokuwa zikiwakabili walimu, hususan ucheleweshwaji wa madaraja na malipo ya baadhi ya stahiki.

“Kwa sasa hakuna kero za walimu kuhusu ucheleweshwaji wa madaraja kwa sababu walimu wote waliokuwa na sifa kwa mujibu wa miongozo walipandishwa kwa wakati,” amesema.

Ameongeza kuwa Serikali imelipa jumla ya shilingi 304,728,000 za malimbikizo ya mishahara kwa walimu katika wilaya hiyo, hatua ambayo imepunguza malalamiko na kuongeza utulivu kazini.

Pia amesema malipo ya fedha za likizo yameboreshwa ambapo kwa sasa walimu wanaweza kuomba likizo zao kupitia mfumo wa kielektroniki wa e-Watumishi, jambo linalorahisisha utoaji wa huduma na kupunguza urasimu katika kushughulikia masuala ya kiutumishi.

Kwa upande wa kuimarisha nidhamu na maadili ya utumishi, Bi. Msangi amesema miongozo mbalimbali iliyotolewa kwa walimu imechangia kuwasaidia kuelewa wajibu wao na kujiepusha na makosa yanayoweza kuhatarisha ajira zao.

Amesema tofauti na kipindi cha nyuma, kwa sasa walimu wanapatiwa



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Hai, Bi. Sophia Abdallah Msangi akiendelea kutekeleza majukumu ofisini kwake hivi karibuni.

mafunzo na elimu kuhusu Sheria, Taratibu na Kanuni za Utumishi wa Umma, hususan kwa walimu wapya wanaoingia kazini.

Katika kuhakikisha walimu wanapata uelewa wa kutosha kuhusu masuala ya kiutumishi, Ofisi ya TSC Wilaya ya Hai imekuwa ikitumia mbinu mbalimbali ikiwemo kufanya vikao na ziara za kikazi shuleni kwa kushirikiana na wadau wa elimu.

Bi. Msangi amesema katika mwaka wa fedha 2023/2024, ofisi hiyo ilifanikiwa kutembelea shule zote za Msingi na Sekondari katika wilaya ya Hai kwa lengo la kufuatilia changamoto za walimu pamoja na kutoa elimu kuhusu Sheria, Taratibu na Kanuni za utumishi.

Ameongeza kuwa wakati mwingine walimu wakuu wa shule huomba ofisi ya TSC ifike shuleni ili kutoa elimu kwa walimu kuhusu masuala ya kiutumishi na maadili ya kazi.

“Wakati mwingine walimu wakuu wanatuomba tufike shuleni kuzungumza na walimu wao kuhusu masuala ya utumishi na maadili ya kazi. Hata wiki iliyopita tulikwenda katika moja ya shule na kuwapatia walimu elimu ili kuwasaidia kuelewa zaidi wajibu wao,” amesema.

TSC HAI YABAINISHA MAFANIKIO KATIKA USIMAMIZI WA UTUMISHI WA WALIMU



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Hai, Bi. Sophia Abdallah Msangi akiendelea kutekeleza majukumu ofisini kwake hivi karibuni.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Hai, Bi. Sophia Abdallah Msangi (wa pili kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wengine wa Tume katika wilaya hiyo.

MIUNDOMBINU BORA NA MATUMIZI YA TEHAMA YACHOCHEA YAWA MOTISHA KWA WALIMU NA WANAFUNZI

Na Mwandishi Wetu – Moshi.

Madarasa mapya, vifaa vya kufundishia, na matumizi ya mifumo ya TEHAMA yameendelea kuibua ari mpya miongoni mwa walimu na wanafunzi, jambo linaloashiria mafanikio makubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuboresha sekta ya elimu. Hii ni kauli ya walimu kutoka shule za msingi na sekondari ambao wameridhishwa na jitihada za Serikali katika kuboresha mazingira ya kazi na ufanisi wa ufundishaji.

Mwalimu wa Shule ya Sekondari Kiusa, Joel Samwel Mollel, amesema maboresho katika maslahi ya walimu yameongezamotishayakazi. "Jitihada zimekuwa nzuri na zimepelekea uboreshaji wa maslahi ya walimu. Malalamiko mengi yamefanyiwa kazi na mishahara inalipwa kwa wakati. Walimu wengi pia wamepandishwa madaraja kwa wakati isipokuwa pale mtu anapokuwa na changamoto maalum," alisema Mwl. Mollel.

Kwa upande wa mafanikio ya kivitendo, Mwalimu wa Shule



Mwl. Stephen Isaya Ndosi wa Shule ya Msingi Mwenge iliyoopo Wilaya ya Moshi akieleza mafanikio ya mitaala mipya na uboreshaji wa miundombinu inavyoongeza morali ya utendaji kazi kwa walimu.

ya Msingi Mwenge iliyoopo Wilaya ya Moshi, Stephen Isaya Ndosi, amesema uboreshaji wa miundombinu ya shule na mitaala mipya umeleta mabadiliko makubwa katika ujifunzaji.

"Mitaala mipya inawawezesha wanafunzi kujifunza kwa vitendo na kwa kina zaidi. Pia, matumizi ya mifumo ya Tehama katika shughuli za kila siku yameongeza ufanisi wetu katika kufundisha na kusimamia shule," alisema Mwl. Ndosi.

Walimu hao wamesema mifumo ya kidijitali katika masuala ya utumishi imesaidia kupunguza matumizi ya karatasi na muda wa kushughulikia nyaraka, ingawa changamoto ya mtandao bado ipo katika maeneo ya vijijini. Aidha, uboreshaji wa madarasa na vitabu pamoja na uwepo wa umeme madarasani umeongeza hamasa ya walimu na wanafunzi, ikiwapa walimu mazingira rafiki ya kufundisha na wanafunzi fursa ya kujifunza vizuri hata wakati wa mawingu.

Mitaala mipya pia imeweka mwanafunzi kama mhusika mkuu wa ujifunzaji, ambapo wanashirikishwa

zaidi katika tafiti, maswali ya kina, na shughuli za vitendo. "Mtaala mpya umeleta mabadiliko chanya. Wanafunzi sasa wanakuwa wahusika wakuu wa ujifunzaji na tunawapa nafasi ya kuonesha ubunifu," amesema Mwl. Mollel. Hata hivyo, walimu wanasema bado wanahitaji mafunzo zaidi ili kutumia kikamilifu mitaala na teknolojia mpya.

Aidha, walimu hao wamesema miongozo ya utumishi waliyopewa imewasaidia kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu, kuimarisha nidhamu na uwajibikaji kazini. "Miongozo hiyo inatupa dira ya jinsi ya kuishi na kufanya kazi kama walimu, kuanzia masuala ya mavazi, ushirikiano kazini hadi uwajibikaji katika majukumu yetu," alisema Mwl. Mollel.

Kwa ujumla, walimu wanapendekeza serikali kuendelea kuimarisha miundombinu, kutoa mafunzo ya mara kwa mara, na kuhakikisha teknolojia na mitaala mipya zinatumiwa kikamilifu, ili kuendeleza mafanikio ya sekta ya elimu kwa manufaa ya walimu na wanafunzi.



Mwl. Stephen Isaya Ndosi wa Shule ya Msingi Mwenge iliyoopo Wilaya ya Moshi akisoma kitabu kinachohusu maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu.



Mwl. Joel Samwel Mollel wa Shule ya Sekondari Kiusa akishirikisha uzoefu wake kuhusu ufanisi wa mifumo ya TEHAMA na usimamizi wa maslahi ya walimu shuleni.

MIONGOZO YA TSC YAIMARISHA USIMAMIZI WA NIDHAMU KWA WALIMU WILAYA YA KARATU

Na Mwandishi Wetu – Karatu

Miongozo mbalimbali iliyotolewa na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeanza kuleta mabadiliko chanya katika usimamizi wa nidhamu kwa walimu katika Wilaya ya Karatu, ambapo Wakuu wa Shule wameanza kuelewa vizuri mipaka ya mamlaka yao katika kuchukua hatua za kinidhamu kwa walimu wanaokiuka sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Karatu, Mwl. Stephano E. Mosha, wakati wa mahojiano na Afisa Habari kutoka Makao Makuu ya TSC kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuimarisha usimamizi wa walimu kupitia Tume hiyo.

Alisema kabla ya utoaji wa elimu na miongozo hiyo, baadhi ya Wakuu wa Shule walikuwa wakichukua hatua za kinidhamu hata kwa makosa makubwa ambayo kisheria hayapo ndani ya mamlaka yao, hali iliyokuwa ikisababisha changamoto katika utekelezaji wa taratibu sahihi za kinidhamu.

“Tunaishukuru Serikali kwa kuwezesha upatikanaji wa miongozo mbalimbali ikiwemo Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu wanaoingia katika utumishi wa umma. Miongozo hii imewasaidia siyo walimu wapya tu, bali hata walimu waliopo kazini pamoja na Wakuu wa Shule kuelewa majukumu yao na kuzingatia sheria na kanuni za utumishi,” alisema Mwl. Mosha.

Alieleza kuwa matokeo ya utekelezaji wa miongozo hiyo yameanza kuonekana ambapo idadi ya mashauri ya nidhamu kwa walimu imepungua kutoka mashauri 26 mwaka 2021 hadi mashauri 10 mwaka 2025 katika Wilaya ya Karatu.

Mbali na kuimarisha nidhamu, Serikali pia imeendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa walimu katika wilaya hiyo. Mwl. Mosha alisema kuwa kati ya mwaka 2021 hadi 2025, jumla ya walimu 2,420 wamepandishwa madaraja, ambapo walimu wa shule za msingi ni 1,584 na walimu wa shule za sekondari ni 836.

Aidha, katika kipindi hicho Serikali imeajiri walimu 353 katika wilaya hiyo hatua iliyosaidia kupunguza mzigo wa kufundisha kwa walimu pamoja na idadi kubwa ya wanafunzi darasani.

Katika kuimarisha miundombinu ya elimu, Serikali pia imejenga shule mpya ya Sekondari ya Patrick Qorro kwa gharama ya shilingi milioni 664.2, ambapo kupitia mradi wa SEQUIP imetoa shilingi milioni 584.2 huku Halmashauri ikichangia shilingi milioni 80 kutoka mapato ya ndani.

Mwl. Mosha alisema ujenzi wa shule hiyo umesaidia kupunguza umbali kwa wanafunzi waliokuwa wakitembea umbali mrefu kwenda kusoma katika Shule za Sekondari za Mlimani Sumawe na Ganako pamoja na kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani.

Aliongeza kuwa matumizi ya mifumo ya kidijitali kama Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Walimu (TSCMIS) yamerahisisha utendaji kazi kwa Makatibu Wasaidizi wa Wilaya hususan katika usajili wa walimu wapya na utoaji wa barua mbalimbali za kiutumishi.

Katika hatua nyingine, Mwl. Mosha alisema



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Karatu Bw. Stephano Mosha akizungumza na Afisa Habari kutoka Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka TSC Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa upande wa Tume.

Halmashauri ya Wilaya ya Karatu imetoa kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya TSC ya Wilaya hiyo ili kuboresha utoaji wa huduma kwa walimu.

“Tunaishukuru Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu kwa kutupatia kiwanja kilichopo Karatu mjini karibu na taasisi nyingine za Serikali kama Mahakama ya Wilaya na TAKUKURU. Hivi sasa taratibu za hati miliki tayari zimekamili kupitia Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Arusha,” alisema.

Kwa upande wao, baadhi ya Wakuu wa Shule katika Wilaya ya Karatu wamesema elimu inayotolewa kuhusu sheria na kanuni za utumishi imewasaidia kusimamia walimu kwa njia shirikishi na kuzuia migogoro isiyo ya lazima kazini.

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Mlimani Sumawe, Mwl. Vitalis Duwe, alisema katika uongozi wake amekuwa akitumia zaidi ushauri na maelekezo badala ya adhabu kali ili kuwasaidia walimu kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia taratibu za utumishi.

Naye Mkuu wa Shule ya Msingi Sumawe, Mwl. Bonaventura Bura, alisema ushirikishwaji wa walimu katika maamuzi ya shule umechangia kuimarisha nidhamu na kuepusha mashauri ya kinidhamu kwa walimu.

Kwa upande wao, baadhi ya walimu wameipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuendelea kuboresha mazingira ya kazi kupitia kupandishwa madaraja kwa wakati, ulipaji wa stahiki pamoja na uwekezaji katika miundombinu ya elimu na matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) shuleni.

Walimu hao walisema hatua hizo zimeongeza motisha kwa walimu na kuchangia kuimarika kwa ufaulu wa wanafunzi katika shule mbalimbali za Wilaya ya Karatu.

MIONGOZO YA TSC YAIMARISHA USIMAMIZI WA NIDHAMU KWA WALIMU WILAYA YA KARATU



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Karatu Bw. Stephano Mosha akizungumza na Afisa Habari kutoka Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka TSC Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa upande wa Tume.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Karatu Bw. Stephano Mosha akionesha Kiwanja cha Tume ambacho wamepatiwa kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi.



Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Mlimani Sumawe Mwl. Vitalis Durwe akiwa katika mahojiano na Afisa Habari kutoka Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka TSC Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa upande wa Shule hiyo.



Mwalimu wa Sekondari ya Mlimani Sumawe Geoffrey Michael Luvino akiwa katika mahojiano na Afisa Habari kutoka Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka TSC Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa upande wa Shule hiyo.

MIONGOZO YA TSC YAIMARISHA USIMAMIZI WA NIDHAMU KWA WALIMU WILAYA YA KARATU



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Karatu Bw. Stephano Mosha akiwa katika picha ya pamoja na walimu wa Shule ya Sekondari ya Mlimani Sumawe hivi karibuni mara mahojiano na na Afisa Habari kutoka Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka TSC Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa upande wa Shule hiyo.



Mkuu wa Shule ya Msingi Sumawe Mwl. Bonventura Bura akiwa katika mahojiano na Afisa Habari kutoka Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka TSC Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa upande wa Shule hiyo.



Mwalimu wa Shule ya Msingi ya Sumawe Bi. Feliciano Justine Kavishe akiwa katika mahojiano na Afisa Habari kutoka Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka TSC Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa upande wa Shule hiyo.

MIONGOZO YA TSC YAIMARISHA USIMAMIZI WA NIDHAMU KWA WALIMU WILAYA YA KARATU



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Karatu Bw. Stephano Mosha akiwa katika picha ya pamoja na walimu wa Shule ya Sekondari ya Mlimani Sumarwe hivi karibuni mara mahojiano na na Afisa Habari kutoka Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka TSC Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awwamu ya Sita kwa upande wa Shule hiyo.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Karatu Bw. Stephano Mosha akiwa katika picha ya pamoja na walimu wa Shule ya Msingi ya Sumarwe mara mahojiano na na Afisa Habari kutoka Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kutoka TSC Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awwamu ya Sita kwa upande wa Shule hiyo.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Karatu Bw. Stephano Mosha akiwa katika picha ya pamoja na walimu wa Shule ya Sekondari mpya ya Patrick Qorro mara mahojiano na Afisa Habari kutoka TSC Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awwamu ya Sita kwa upande wa Shule hiyo.

Maboresho ya Serikali ya Awamu ya Sita Yawapa Walimu Motisha Zaidi Kazini

“

Siku hizi walimu wameboreshewa maslahi na tunafurahi kwa kweli. Ukiitisha mkutano wa walimu wakati mwingine tunakosa hata sehemu za kugesha magari kwa sababu walimu wengi sasa wanamiliki magari. Hii inaonesha walimu wamewezesha na maisha yao yameimarika,”

Na Mwandishi Wetu – Hai, Kilimanjaro.

Maboresho yanayoendelea kufanywa na Serikali ya Awamu ya Sita katika sekta ya elimu yameendelea kuleta matokeo chanya kwa walimu na wanafunzi, huku yakiongeza ari ya walimu katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Hayo yameelezwa na Mkuu wa Shule ya Sekondari Hai mkoani Kilimanjaro, Mwl. Alex John Warioba, katika mahojiano maalum ambapo amesema tangu Serikali ya Awamu ya Sita iingie madarakani mwezi Machi mwaka 2021 kumekuwa na maboresho makubwa katika maslahi ya walimu pamoja na mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

Amesema moja ya maboresho yaliyowapa faraja walimu ni kuimarika kwa masuala ya upandishwaji vyeo na mishahara ambayo hapo awali yalikuwa yakisababisha changamoto kwa walimu wengi.

“Tangu Awamu ya Sita iingie madarakani walimu wanafanya kazi kwa utulivu zaidi. Zamani kulikuwa na changamoto za kupanda madaraja, lakini sasa walimu wanapandishwa kwa wakati na hata wale waliocheleweshwa wamelipwa stahiki zao. Hili limetupa faraja kubwa sana,” amesema.

Ameongeza kuwa kwa sasa mwalimu anapopandishwa cheo hupata mishahara wake mpya kwa wakati tofauti na ilivyokuwa zamani ambapo walimu walilazimika kusubiri kwa muda mrefu kupata stahiki zao.

“Kinachotufurahisha zaidi ni kupanda cheo na hapo hapo unapata mishahara mpya. Huko nyuma tulikuwa na madai mengi sana, lakini sasa hali imebadilika na imetupa motisha kubwa kazini,” amesema.

Mwl. Warioba amesema maboresho ya maslahi ya walimu pia yamechangia kubadilisha maisha ya walimu wengi kwa kuwawezesha kujikimu kiuchumi na kufanya uwekezaji katika shughuli mbalimbali.

“Siku hizi walimu wameboreshewa maslahi na tunafurahi kwa kweli. Ukiitisha mkutano wa walimu wakati mwingine tunakosa hata sehemu za kugesha magari kwa sababu walimu wengi sasa wanamiliki magari. Hii inaonesha walimu wamewezesha na maisha yao yameimarika,” alisema.

Mbali na maslahi ya walimu, amesema Serikali imefanya kazi kubwa katika kuboresha miundombinu ya shule kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo ya elimu, hatua ambayo imeongeza mazingira bora ya kujifunzia na kufundishia.

Amesema miradi hiyo imesaidia kujenga madarasa mapya, kukarabati majengo ya zamani pamoja na kujenga shule mpya.

“Miundombinu ya shule imeboreshwa sana. Madarasa

mapya yanajengwa, mengine yanakarabatiwa na hata shule mpya zimejengwa. Tofauti na zamani ambapo wanafunzi walikuwa wanachaguliwa ndipo madarasa yajengwe, sasa madarasa yanajengwa mapema na yanakuwa tayari kusubiri wanafunzi,” amesema.

Kwa mujibu wa Mwl. Warioba, uboreshaji huo wa miundombinu umechangia kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani na kuboresha mazingira ya ujifunzaji.



Mkuu wa Shule ya Sekondari Hai mkoani Kilimanjaro, Mwl. Alex John Warioba akizungumza namna walimu wanavyoridhishwa na juhudi za Serikali katika kuboresha Elimu.

Maboresho ya Serikali ya Awamu ya Sita Yawapa Walimu Motisha Zaidi Kazini

Amesema kwa sasa wanafunzi wengi wanapata vitabu vya kujifunzia kwa urahisi na vifaa vya maabara vinaendelea kupelekwa shuleni, hali inayochangia kuboresha ufundishaji wa masomo ya sayansi.

"Kwa sasa msongamano wa wanafunzi darasani umepungua na vitabu vimeongezeka kiasi kwamba wanafunzi wengi wanapata vitabu vya kujifunzia. Pia vifaa vya maabara vinaendelea kuletwa na baadhi ya shule sasa zina maabara hadi nne," amesema.

Aidha, amesema ujenzi wa nyumba za walimu umechangia kupunguza changamoto ya walimu kupanga nyumba mbali na vituo vya kazi, jambo linalowawezesha kutumia muda mwingi zaidi kujiandaa kwa ajili ya kufundisha.

Ameeleza kuwa maboresho hayo yamechangia pia kupungua kwa utoro kwa wanafunzi na kuongezeka kwa ufaulu wa kitaaluma.

"Zamani tulikuwa tunaona wanafunzi wengi wanapata sifuri katika mitihani, lakini kwa sasa hali imebadilika sana. Sifuri ni nadra kwa sababu mazingira ya kujifunzia yameboreshwa na wanafunzi wanapata vifaa vinavyowasaidia kujifunza vizuri," amesema.

Akizungumzia matumizi ya mifumo ya TEHAMA, Mwl. Warioba amesema mifumo hiyo imeleta mapinduzi katika utendaji kazi wa walimu na watendaji wa shule.

"Mifumo imerahisisha sana utendaji kazi. Sasa tunaweza kujitathmini kupitia mifumo, kutunza takwimu za shule kwa usahihi na hata kushughulikia masuala ya kiutumishi bila kulazimika kutoka vituoni," amesema.

Ameongeza kuwa hata huduma kama maombi ya mikopo, likizo na masuala mengine ya kiutumishi sasa yanafanyika kwa kutumia mifumo ya kielektroniki.

Kuhusu utekelezaji wa mitaala mipya ya elimu, Mwl. Warioba amesema mabadiliko hayo yanaendelea kuleta matokeo chanya hasa katika kuimarisha masomo ya amali yanayolenga kuwapa wanafunzi ujuzi wa vitendo.

"Tumeanza kuona walimu wa masomo ya amali kama biashara na lishe wakiongezeka. Hii ni hatua nzuri, lakini bado kuna haja ya kuendelea kuboresha miundombinu ya masomo ya vitendo katika baadhi ya shule," amesema.

Aidha, amesema miongozo mbalimbali inayotolewa kwa walimu imekuwa msaada mkubwa katika kuwawezesha kuelewa na kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za utumishi wa umma.

"Miongozo hiyo inatukumbusha wajibu wetu kama walimu. Inaeleza wazi nini kinapaswa kufanywa na matokeo yake kama mwalimu hatatimiza wajibu wake. Hivyo walimu wengi sasa wanazingatia maadili ya kazi na kutekeleza majukumu yao ipasavyo," amesema.

Kwa ujumla, Mwl. Warioba amesema maboresho yanayoendelea kufanywa na Serikali katika sekta ya elimu yamewapa walimu utulivu na motisha zaidi ya kuendelea kutoa huduma bora ya elimu kwa wanafunzi nchini.



Mkuu wa Shule ya Sekondari Hai mkoani Kilimanjaro, Mwl. Alex John Warioba akizungumza namna walimu wanavyoridhishwa na juhudi za Serikali katika kuboresha Elimu.

BARAZA LA WAFANYAKAZI TSC LAPITIA UTEKELEZAJI NA MAKADIRIO YA BAJETI YA TUME KWA MWAKA 2026/2027

Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akifungua mkutano wa Baraza uliofanyika tarehe 12 Machi, 2026 katika ukumbi wa Mabele jijini Dodoma

Na Mwandishi Wetu

Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) limekutana kujadili na kupitia utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na makadirio ya bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 kwa lengo la kuimarisha ufanisi wa utendaji kazi wa Tume hiyo.

Akifungua mkutano huo, Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi aliwataka wajumbe kushiriki kikamilifu katika mijadala ya masuala ya bajeti ili kuhakikisha mipango ya Tume inatekelezwa kwa ufanisi na kwa kuzingatia malengo yaliyowekwa. Alisisitiza umuhimu wa ushirikiano miongoni mwa watumishi katika kufanikisha majukumu ya Tume ya kusimamia masuala ya utumishi wa walimu nchini.

Katika neno la utangulizi, Katibu wa Baraza la Wafanyakazi, Bw. Nuhu Mlekwa, alieleza kuwa mkutano huo ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa taratibu za usimamizi wa rasilimali za umma, ambapo wajumbe hupata fursa ya kupitia utekelezaji wa bajeti ya mwaka unaoendelea na kutoa maoni kuhusu makadirio ya bajeti ya mwaka ujao.

Aidha, wajumbe wa mkutano huo walipata wasilisho kutoka kwa Afisa Uchumi wa Tume, Bi. Zaitun Ramadhani, ambaye aliwasilisha mada kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Tume kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Katika wasilisho lake alieleza mafanikio yaliyopatikana pamoja na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa bajeti hiyo.

Kwa upande mwingine, Afisa Uchumi Mkuu wa Tume, Bw. Elia Malaki, aliwasilisha mada kuhusu makadirio ya bajeti ya Tume kwa mwaka wa fedha 2026/2027, akibainisha maeneo ya kipaumbele yatakayowezesha

Tume kuendelea kuboresha huduma zake kwa walimu na wadau wengine wa sekta ya elimu.

Wajumbe wa Baraza walipata fursa ya kujadili mada zilizowasilishwa na kutoa mapendekezo mbalimbali yaliyolenga kuboresha mipango ya Tume na kuhakikisha rasilimali za umma zinatumiwa kwa ufanisi zaidi.

Mkutano huo ulihitimishwa kwa wajumbe kusisitizwa umuhimu wa uwazi, uwajibikaji na ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu ya Tume ili kuendelea kutoa huduma bora kwa walimu na kuchangia maendeleo ya sekta ya elimu nchini.



Katibu wa Baraza la Wafanyakazi la TSC, Bw. Nuhu Mlekwa, akitoa neno la utangulizi wakati wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi uliofanyika tarehe 12 Machi, 2026 jijini Dodoma.

BARAZA LA WAFANYAKAZI TSC LAPITIA UTEKELEZAJI NA MAKADIRIO YA BAJETI YA TUME KWA MWAKA 2026/2027

Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akifungua mkutano wa Baraza uliofanyika tarehe 12 Machi, 2026 katika ukumbi wa Mabele jijini Dodoma



Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi la TSC wakiimba wimbo wa mshikamano daima wakati wa Mkutano wa Baraza hilo uliofanyika tarehe 12 Machi, 2026 jijini Dodoma.




Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi la TSC wakifuatilia kwa makini mjadala na mada zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Baraza hilo uliofanyika tarehe 12 Machi, 2026 jijini Dodoma.

BARAZA LA WAFANYAKAZI TSC LAPITIA UTEKELEZAJI NA MAKADIRIO YA BAJETI YA TUME KWA MWAKA 2026/2027



Afisa Uchumi wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Bi. Zaitun Ramadhani, akiwasilisha mada kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Tume kwa mwaka wa fedha 2025/2026.



Afisa Uchumi Mkuu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Bw. Elia Malaki, akiwasilisha mada kuhusu makadirio ya bajeti ya Tume kwa mwaka wa fedha 2026/2027.



Mkurugenzi Msaidizi wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu wa Tume ya Utumishi wa Walimu akiwasilisha mada kwenye Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu uliofanyika tarehe 12 Machi, 2026 jijini Dodoma.



Mwenyekiti wa TUGHE Tawzi la Tume ya Utumishi wa Walimu, Bw. Francis Gwankisa akichangia hoja wakati wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu uliofanyika tarehe 12 Machi, 2026 jijini Dodoma.

BARAZA LA WAFANYAKAZI TSC LAPITIA UTEKELEZAJI NA MAKADIRIO YA BAJETI YA TUME KWA MWAKA 2026/2027

Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi la TSC wakifuatilia kwa makini mijadala na mada zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Baraza hilo uliofanyika tarehe 12 Machi, 2026 jijini Dodoma.



Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya washiriki wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la Tume tarehe 12 Machi, 2026 jijini Dodoma.

TSC ARUMERU YAIMARISHA UTOAJI ELIMU KUHUSU SHERIA NA MAADILI YA UTUMISHI KWA WALIMU

Na Mwandishi Wetu – Arumeru

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Arumeru imeendelea kuimarisha utoaji wa elimu kwa walimu kuhusu sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia utumishi wao ili kuongeza uelewa na kuimarisha nidhamu katika sekta ya elimu.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Arumeru, Bi. Zeituni Kinkwerema, wakati wa mahojiano na Afisa Habari kutoka Kitengo cha Mawasiliano Serikalini yaliyofanyika ofisini kwake.

Bi. Kinkwerema alisema kuwa TSC imekuwa ikiendesha ziara katika shule mbalimbali za msingi na sekondari kwa lengo la kuwajengea walimu uelewa kuhusu masuala ya ajira, maadili na kanuni za utumishi wa umma.

Alisema kuwa katika ziara hizo pia wamekuwa wakikutana na maafisa elimu katika ngazi mbalimbali ambao hushiriki katika mijadala kuhusu namna bora ya kuimarisha uelewa wa walimu juu ya sheria na taratibu zinazowaongoza katika utekelezaji wa majukumu yao.

Aidha, alisema Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kushughulikia changamoto mbalimbali zilizokuwa zikiwakabili walimu katika Wilaya ya Arumeru, ikiwemo ucheleweshaji wa upandishwaji madaraja, kubadilishiwa miundo ya utumishi pamoja na ulipaji wa madeni ya walimu.

Kwa mujibu wa Bi. Kinkwerema, kuanzia mwaka 2021 hadi 2025 jumla ya walimu 8,135 wamepandishwa madaraja katika Wilaya ya Arumeru, huku walimu 501 wakibadilishiwa miundo ya utumishi baada ya kujiendeleza kielimu.

Aliongeza kuwa katika kipindi hicho pia walimu 385 wameajiriwa katika wilaya hiyo ili kuimarisha utoaji wa huduma ya elimu katika shule za msingi na sekondari.

Bi. Kinkwerema alisema kuwa katika kuhakikisha kero na changamoto za walimu zinatatuliwa kwa wakati, TSC imekuwa ikishirikiana na ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri zote mbili za Wilaya



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Arumeru Bi. Zeituni Kinkwerema akiwa katika mahojiano na Afisa Habari kutoka Kitengo cha Mawasiliano Serikalini ofisini kwake hivi karibuni kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Tume kwa Wilaya hiyo.

ya Arumeru kuandaa kliniki maalum za kusikiliza na kutatua changamoto zinazowakabili walimu.

Alisema kuwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 TSC kwa kushirikiana na wadau wengine iliweza kufika katika shule 28 na kutoa elimu kwa walimu 405 kuhusu sheria, kanuni na taratibu za utumishi wao.

Aidha, kwa mwaka wa fedha 2024/2025 TSC ilifanya ziara katika shule 58 na kufikisha elimu kwa walimu 828 wa shule za msingi na sekondari katika wilaya hiyo, huku hadi kufikia Machi 2026 ikiwa tayari imewafikia walimu 558 katika kata 18.

Bi. Kinkwerema aliongeza kuwa TSC imeendelea kutumia mikutano

na vikao vinavyoandaliwa na wakurugenzi wa halmashauri kutoa elimu kuhusu masuala ya ajira, maadili na uzingatiaji wa sheria za utumishi kwa walimu wa umma.

Aidha, alisema TSC imekuwa ikishirikiana na ofisi za wakurugenzi kuwashauri walimu wenye changamoto za kitabia, ikiwemo matumizi mabaya ya pombe yanayosababisha utoro kazini, na kuwapeleka katika vituo vya ushauri nasaha ili kuwasaidia kurekebisha tabia zao.

Alisema kuwa hatua hizo zimechangia kupunguza matukio ya walimu kuingia katika makosa ya kinidhamu na hivyo kuimarisha utoaji wa huduma ya elimu katika Wilaya ya Arumeru.

WALIMU WA WILAYA YA ARUMERU WAISHUKURU SERIKALI KWA UTATUZI WA CHANGAMOTO ZAO

Na Mwandishi Wetu-Arumeru

Baadhi ya Walimu wa Wilaya ya Arumeru wameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusikiliza kilio chao na kutatua changamoto ambazo zilikuwa zikiwakatisha tamaa katika utekelezaji wa makujumu yao.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Sokoni II Mwl. Eliakimu Singo alisema kuwa Serikali imejitahidi kuhakikisha kuwa maslahi ya walimu yanashughulikiwa na kutoa kero zilikuwepo kwa muda mrefu zikiwemo za walimu kuwa katika daraja moja kwa muda mrefu, kulipwa madeni yao yakiwemo ya mapunjo ya mishahara na likizo.

Aliongeza kuwa hivi sasa Serikali ya Awamu ya Sita imekuwa ikilipa mishahara kwa wakati bila kupitiliza, jambo ambalo limewafurahisha walimu na kuwaongezea morali ya kutekeleza majukumu yao.

Mwl. Singo alisema kupitia Serikali wameweza kupata wadau ambao wamewapatia vifaa vya matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ambavyo wamekuwa wakiutumia kurahisisha utekelezaji wa majukumu yao yakiwemo ya kutuma taarifa kwa wakati na kuandaa masomo na mitihani.

Mwalimu Geoffrey Mvamba alisema kuwa Serikali kupitia Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu



Mkuu wa Shule ya Sekondari Sokoni II Mwl. Eliakimu Singo akiwa katika mahojiano na Afisa Habari kutoka Kitengo cha Mawasiliano Serikalini cha Tume ya Utumishi wa Walimu ofisini kwake hivi karibuni kuhusu mafanikio ya Serikali.

Wilaya ya Arumeru imewasaidia kuhakikisha kuwa walimu wote waliokuwa wanachangamoto katika upandishwaji madaraja wanapanda kwa msrereko.

Alisema kuwa hata walimu waliokuwa masomoni ambapo siku za nyuma walipokuwa wakirudi walikuwa wakikaa muda mrefu bila kubadilishwa muundo. Kwa sasa wanabadilishiwa kwa wakati na hukuna kutumikia Muundo kwani wanafanyiwa Data Cleaning na kupewa muundo unaoendana na tarehe ya daraja la mwisho hivyo kufurahia utumishi wao.

Aidha, Mwl. Mvamba aliishukuru Ofisi ya TSC Wilaya ya Arumeru kwa kuwa karibu na walimu na kila wakati kuwaelimisha kuhusu maadili na Sheria, Kanuni na Taratibu zinazowasimilia katika utumishi wao na ule wa umma.

Aliiomba Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuendelea kuwajengea uwezo walimu katika matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ili wawe mahiri katika ufundishaji kulingana na maendeleo yanayoendelea duniani ambapo TEHAMA imetawala nyanja nyingi.

Mwalimu Irene Frank Lyimo aliishukuru Serikali kwa kusikia maombi ya walimu na watumishi ya nyongeza za mishahara na hatimaye kuwaongezea ambapo


umewaongezea morali kwenye utekelezaji wa majukumu yao.

Aliongeza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imesaidia kuondoa changamoto zilizokuwepo kwa muda mrefu ikiwemo walimu kutopandishwa madaraja, kuwa na madeni ya mapunjo na nauli wakati wa likizo. Kwa sasa madeni yamelipwa na likizo zinalipwa kwa wakati.

Aidha, Mwl. Irene alisema kuwa uanzishwaji wa Mfumo wa Upimaji Utendaji wa Majukumu wa ESS umewasaidia watumishi kufunguliwa fursa mbalimbali ikiwemo za kuokoa muda katika utumaji wa taarifa, kupata mikopo bila ukiritimba na kuwapa watumishi machaguo mengi ya kutafuta mikopo kwenye benki mbalimbali na kuongeza faragha kwa mtumishi.

Alisema kuwa kuhusu elimu, Serikali imejitahidi kuwekeza katika kuhakikisha kunakuwepo na vitabu vya kiada na ziada vya kutosha ambapo katika Sekondari ya Sokoni II kila mwanafunzi anatumia kitabu chake bila kuchangia na mwenzake.

Mwl. Irene alisema kuwa kwa upande wa matumizi ya teknolojia ya habari na Mawasiliano katika Shule hiyo yamesaidia kurahisisha ufunndishaji ambapo kuna wakati wanatumia picha mjengefu (Video) na Projector kuwaelevesha wanafunzi katika baadhi ya mada.



Mwalimu wa Shule ya Sekondari Sokoni II Mwl. Geoffrey Mvamba akiwa katika mahojiano na Afisa Habari kutoka Kitengo cha Mawasiliano Serikalini cha Tume ya Utumishi wa Walimu hivi karibuni kuhusu mafanikio ya Serikali.



Mwalimu wa Shule ya Sekondari Sokoni II Mwl. Irene Lyimo akiwa katika mahojiano na Afisa Habari kutoka Kitengo cha Mawasiliano Serikalini cha Tume ya Utumishi wa Walimu hivi karibuni kuhusu mafanikio ya Serikali.

WALIMU WA WILAYA YA ARUMERU WAISHUKURU SERIKALI KWA UTATUZI WA CHANGAMOTO ZAO



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu(TSC) Wilaya ya Arumeru Bi Zeituni Kinkwerema (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Maafisa wa Tume mara mahojiano na Afisa Habari kutoka Kitengo cha Mawasiliano Serikalini ofisini kwake hivi karibuni kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Tume kwa Wilaya hiyo.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu(TSC) Wilaya ya Arumeru Bi Zeituni Kinkwerema (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na mtumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Arumeru Bw. Evarist P. Kimaro (wa kwanza kushoto) pamoja na Walimu wa Shule ya Sekondari ya Sokoni II

TSC MONDULI YAENDELEA KUTOA ELIMU KWA WALIMU KUHUSU SHERIA ZA UTUMISHI

Na Mwandishi Wetu – Monduli

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Monduli imeendelea kutekeleza ziara katika shule mbalimbali za umma za msingi na sekondari kwa lengo la kutoa elimu kwa walimu kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utumishi wao, hatua inayolenga kuimarisha nidhamu kazini.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa Ofisi ya TSC Wilaya ya Monduli, Bw. Hussein Ally, wakati wa mahojiano na Afisa Habari kutoka Makao Makuu ya TSC kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Tume hiyo.

Bw. Ally alisema kuwa katika ziara hizo wamekuwa wakitoa miongozo, vitabu na vipeperushi vinavyoeleza masuala mbalimbali ya ajira na nidhamu kwa walimu ili kuwasaidia kuelewa wajibu wao katika utumishi wa umma.

Aliongeza kuwa utoaji wa elimu

hiyo umeleta matokeo chanya ikilinganishwa na miaka ya nyuma ambapo baadhi ya walimu walikuwa na uelewa mdogo kuhusu makosa yanayoweza kuhatarisha ajira zao. Hali hiyo imechangia kupungua kwa mashauri ya kinidhamu kutoka mashauri 19 yaliyorekodiwa katika kipindi cha mwaka 2023/2024 hadi kufikia mashauri sita katika mwaka 2025/2026.

“Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2025, TSC Wilaya ya Monduli imeendelea kutoa elimu kuhusu masuala ya ajira, maadili na nidhamu kwa walimu walioajiriwa na Serikali, pamoja na kugawa vijitabu na vipeperushi vilivyotolewa na TSC Makao Makuu ili walimu waweze kujisomea na kuongeza uelewa wao kuhusu utumishi wao,” alisema.

Aidha, alisema Serikali kupitia Ofisi ya TSC Wilaya ya Monduli imeendelea kushughulikiachangamotombalimbali za walimu, ikiwemo ucheleweshaji wa upandishwaji wa vyeo na mabadiliko ya miundo ya utumishi, ambapo hatua

zimechukuliwa kuzitafutia ufumbuzi.

Kwa mujibu wa Bw. Ally, katika kipindi cha mwaka 2022 hadi 2025 jumla ya walimu 1,155 wamepandishwa vyeo, huku walimu 127 wakibadilishiwa miundo ya utumishi baada ya kujiendeleza kielimu.

Alifafanua kuwa kati ya walimu waliopandishwa madaraja, walimu wa shule za msingi ni 713 na wa shule za sekondari ni 442. Kwa upande wa walimu waliobadilishiwa miundo ya utumishi, walimu wa shule za msingi ni 103 na wa sekondari ni 24.

Bw. Ally pia aliishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi wa Tume katika Wilaya ya Monduli kuhusu masuala ya nidhamu, ajira na maendeleo ya walimu, jambo linalowasaidia kutoa huduma bora kwa walimu.

Kwa upande wao, baadhi ya walimu wa Shule ya Sekondari ya Irkisongo wamesema miongozo inayotolewa na Serikali kupitia TSC imewasaidia kuelewa vizuri sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa walimu na hivyo kuwaepusha kuingia katika makosa ya kinidhamu.

Walimu hao walisema miongozo hiyo imewawezesha kutambua haki na wajibu wao pamoja na mipaka ya majukumu yao katika utumishi wa umma.

“Miongozo inayotolewa ni muhimu sana kwani inatoa mwanga kuhusu wajibu wa walimu katika utumishi wa umma, taratibu za kazi pamoja na haki na mipaka ya majukumu yetu,” walisema.

Aidha, walimu hao waliipongeza Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuboresha maslahi ya walimu, hususan kwa kuhakikisha mishahara inalipwa kwa wakati pamoja na kuboresha miundombinu ya shule.

Walisema maboresho ya miundombinu ya shule yamechangia kuongeza ari na ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuweka mazingira bora kwa walimu na wanafunzi.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Ofisi ya TSC Wilaya ya Monduli, Bw. Hussein Ally, akiwa katika mahojiano na Afisa Habari kutoka Makao Makuu ya TSC kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Tume hiyo.

TSC MONDULI YAENDELEA KUTOA ELIMU KWA WALIMU KUHUSU SHERIA ZA UTUMISHI



Kaimu Katibu Msaidizi wa Ofisi ya TSC Wilaya ya Monduli, Bw. Hussein Ally, akiwa katika mahojiano na Afisa Habari kutoka Makao Makuu ya TSC kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Tume hiyo.



Bw. Hussein Ally akizungumza na walimu wa Shule ya Sekondari ya Irkisongo wakati wa ziara ya kutoa elimu kuhusu masuala ya ajira na nidhamu kwa walimu.

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Irkisongo, Bi. Nyanyama Bwire Chiremeji, akitoa maelezo wakati wa ziara ya Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Monduli.



Baadhi ya walimu wa Shule ya Sekondari ya Irkisongo wakimsikiliza Bw. Hussein Ally (hayupo pichani) wakati wa utoaji wa elimu kuhusu ajira na nidhamu kwa walimu.

MIONGOZO YASAIIDIA KUWAJENGEA UWEZO WALIMU WILAYA YA ARUSHA KUEPUKA MASHAURI YA KINIDHAMU

Na Mwandishi Wetu – Arusha

Miongozo mbalimbali iliyotolewa na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeendelea kuwajengea uwezo walimu kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia utumishi wao, hatua iliyosaidia baadhi yao kuepuka makosa ambayo yangesababisha kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Arusha, Bi. Gloria Sailoja, wakati wa mahojiano na Afisa Habari kutoka Makao Makuu ya TSC kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika sekta ya elimu kupitia Tume hiyo.

Bi. Sailoja alisema kuwa utekelezaji wa miongozo hiyo umechangia kupungua kwa idadi ya mashauri ya kinidhamu yanayofunguliwa dhidi ya walimu, ambapo katika robo ya kwanza ya mwaka huu mashauri mawili pekee yalifunguliwa ikilinganishwa na mashauri saba yaliyokuwa yakipokelewa hapo awali.

Alieleza kuwa katika kuhakikisha walimu wanazifahamu sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia utumishi wao, ofisi ya TSC imekuwa ikigawa vitabu vya miongozo mbalimbali pamoja na kutumia mikutano na vikao vinavyoandaliwa na Mkurugenzi wa Halmashauri kutoa elimu kuhusu masuala ya ajira, maadili na uwajibikaji kwa walimu wa umma.

Aidha, alisema kwa kushirikiana na wadau kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, waliweza kufika katika shule 13 na kutoa elimu kwa walimu 673 kuhusu sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa walimu.

Bi. Sailoja aliongeza kuwa katika mwaka wa fedha 2024/2025, ofisi hiyo pia ilifanya ziara ya kikazi katika shule 49 za msingi na sekondari katika Wilaya ya Arusha kwa lengo la kuwapatia walimu elimu kuhusu wajibu wao katika utumishi wa umma.

Alisema hatua hizo zimechangia kuimarika kwa utendaji wa walimu katika Jiji la Arusha, hali iliyosaidia halmashauri hiyo kuendelea kufanya vizuri katika matokeo ya kitaifa ya mitihani, ambapo mwaka 2021 ilishika nafasi ya kwanza na mwaka 2025 pia ikaendelea kushika nafasi ya kwanza.

Katika hatua nyingine, Bi. Sailoja alisema kuwa kuanzia mwaka 2021 hadi 2025, Ofisi ya TSC Jiji la Arusha imefanikiwa kusajili walimu 188 walioajiriwa katika utumishi wa umma, kuwapatia mikataba na barua za ajira pamoja na kuwathibitisha kazini walimu 188 waliomaliza kipindi cha majaribio.

Aliongeza kuwa katika kipindi hicho walimu wameendelea kupandishwa vyeo kwa kuzingatia miongozo iliyotolewa na Tume, ambapo walimu wa shule za msingi 1,137 na walimu wa shule za sekondari 1,081 walipandishwa vyeo, huku walimu 313 wakibadilishiwa miundo ya utumishi baada ya kujiendeleza kielimu.

Aidha, alisema kuwa katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumeshuhudiwa ongezeko la ajira za walimu, kupandishwa kwa vyeo kwa wakati, kulipwa kwa mishahara kwa wakati pamoja na ulipaji wa likizo na madai mbalimbali ya walimu.



**MIONGOZO YAS Aidia Kuwajengea Uwezo Walimu
Wilaya ya Arusha Kuepuka Mashauri ya Kinidhamu**



WALIMU 1,069 WA WILAYA YA LONGIDO WAPANDISHWA VYEO, MASHARITI YA AJIRA YAMEIMARISHWA

Na Mwandishi Wetu- Morogoro

Na Mwandishi Wetu – Longido Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Longido imefanikiwa kuratibu upandishaji vyeo kwa walimu jumla ya 1,069 kati ya mwaka 2021 hadi 2025, ikiwemo walimu 634 wa shule za msingi na 435 wa shule za sekondari.

Hayo yameelezwa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Ofisi ya TSC Wilaya ya Longido, Bw. Boniphace Bitu, wakati wa mahojiano na Afisa Habari kutoka Makao Makuu ya TSC kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa upande wa Tume.

Bw. Bitu aliongeza kuwa katika kipindi hicho, ofisi ya TSC Wilaya ya

Longido pia imefanikiwa kuratibu ubadilishaji wa miundo ya utumishi kwa walimu 78 waliojiendeleza kielimu, kati ya hao walimu wa sekondari ni 21 na walimu wa msingi ni 57.


Aidha, Bw. Bitu alisema kuwa Tume imefanikiwa kuratibu na kutoa mikataba ya kazi na barua za ajira mpya kwa walimu 247 katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2026, huku walimu 172 waliothibitishwa kazini kufikia vigezo vilivyowekwa.

Mafanikio mengine ni pamoja na kuunganisha Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Walimu (TSCMIS), ambao umewezesha Ofisi kusindika taarifa za walimu kwa haraka, kwa usahihi na urahisi zaidi. Mfumo huu pia unarahisisha upatikanaji wa barua za ajira na mikataba ya watumishi

walioko katika utumishi wa umma kwa wakati unaofaa.

Bw. Bitu alibainisha kuwa walimu 80 walioajiriwa mwaka 2025 walipatiwa mafunzo maalumu kupitia Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa walimu wapya, yaliyotolewa na Tume. Mafunzo haya yamesaidia kuwapa walimu uelewa wa utumishi wa ualimu, haki na wajibu wao, pamoja na mambo yanayohitaji kuepukwa ili kutoathiri maadili ya utumishi wa umma.

Aidha, Bw. Bitu alisema kuwa TSC imeendelea kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi kutoa elimu kwa walimu katika shule mbalimbali za umma, hatua ambayo imesaidia kupunguza idadi ya mashauri ya kinidhamu kutoka mashauri 11 mwaka 2024 hadi 2 tu mwaka 2026.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Longido, Bw. Boniphace Bitu (kushoto), akiwa katika mahojiano na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Makao Makuu ya TSC, Bw. Tiganya Vincent (hayupo katika picha), kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa upande wa Tume.

WATUMISHI TSC WACHAGUA VIONGOZI WAPYA SHIMIWI, TUGHE

Na Mwandishi Wetu – Dodoma

Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wamechagua viongozi wapya wa Shirikisho la Michezo la Wizara, Idara Huru na Wakala wa Serikali (SHIMIWI) Tawi la Tume, hatua inayotarajiwa kuimarisha uratibu wa shughuli za michezo pamoja na mshikamano miongoni mwa watumishi wa taasisi hiyo.

Uchaguzi huo uliofanyika Machi 31, 2026 ulisimamiwa na Makamu Mwenyekiti wa SHIMIWI Taifa, Bw. Alqwin Michael Masubo, ambaye alisema viongozi waliochaguliwa watakuwa na jukumu la kuongoza na kusimamia masuala ya michezo ndani ya Tume kwa kipindi cha miaka minne.

Bw. Masubo aliwataka viongozi hao kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi huku wakiendelea kuzingatia wajibu wao wa msingi waliyoajiriwa kuyatekeleza katika taasisi hiyo.

Katika uchaguzi huo, Bw. Muhia Lyatuu alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa SHIMIWI Tawi la Tume ya Utumishi wa Walimu, huku Makamu Mwenyekiti akiwa Bi. Elieth Ntinabo. Nafasi ya Katibu imechukuliwa na Bi. Enid Geoffrey na Katibu Msaidizi ni Bi. Kamunde Kaswezi.

Nafasi ya Mwakilishi wa Mkutano Mkuu wa SHIMIWI Taifa imechukuliwa na Bw. David Igogo, huku Bw. Evans Urassa akichaguliwa kuwa Mhazini.

Wajumbe wa Kamati Tendaji waliochaguliwa ni Bw. Edward Burton, Bi. Verediana Emil, Bw. Gabriel Mbwalala, Bi. Hellen Mchome na Bw. Rajab Kalobo.

Uongozi huo mpya unatarajiwa kuendeleza na kuimarisha ushiriki wa watumishi wa Tume katika michezo mbalimbali chini ya SHIMIWI, hatua itakayochochea afya bora, mshikamano na ufanisi kazini.

Katika hatua nyingine, watumishi wa Tume pia wamechagua viongozi wapya wa Tanzania Union of Government and Health Employees

(TUGHE) Tawi la Tume watakaojaza nafasi za viongozi waliomaliza muda wao wa uongozi.

Katika uchaguzi huo, Bi. Zena Hassan alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Tawi huku Bw. Rajab Kalobo akichaguliwa kuwa Katibu wa Tawi.

Aidha, wajumbe waliochaguliwa kuingia katika Halmashauri Kuu ya TUGHE Tawi ni Bi. Adelina Nyoni, Bw. Gabriel Mbwalala, Bi. Grace Mauki, Bw. Timothy Mtafya, Bi. Judith Shange,

Bw. Nsajigwa Mwakatika, Bw. Theofil Kamugisha na Bw. Lufingo Mng'ong'o. Nafasi ya Mwakilishi wa Vijana imechukuliwa na Bi. Verediana Emil.

Kwa upande wa Kamati ya Wanawake, Bi. Flora Chanda alichaguliwa kuwa Mwenyekiti, Bi. Janeth Lukuwi kuwa Katibu na Bi. Fatuma Hussein kuwa Mweka Hazina. Wajumbe wa kamati hiyo ni Bi. Enid Geoffrey na Bi. Kamunde Kaswezi.



Msimamizi wa Uchaguzi wa Viongozi wa TSC Sports Club ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa SHIMIWI Taifa Bw. Alqwin Michael Masubo (aliyesimama) akitoa mwongozo wa kusimamia uchaguzi wa viongozi wa Tume kwa kipindi cha miaka minne.

MIONGOZO YA SERIKALI YAWAIMARISHA WALIMU WILAYANI TANGANYIKA



Baadhi ya Wafanyakazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiwa katika zoezi la kuwachagua viongozi wao wa TSC Sports Club.



Baadhi ya viongozi wapya wa SHIMIWI Tawi la TSC wakiwa katika picha ya pamoja.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu